

OFISI YA WAZIRI MKUU
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA SENGEREMA
SHULE YA SEKONDARI NYAMPULUKANO



S.L.P. 104

SENGEREMA

Tarehe

SIMU 2590065/0765976281/0767799592/0759766350

Ndugu.....

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE

Ninafurahi kukuarifu kuwa umechaguliwa kuendelea na elimu ya sekondari kidato cha Tano katika shule ya sekondari Nyampulukano. Unapaswa kufika shuleni tarehe..... kabla ya saa 11.00 jioni. Shule ipo umbali wa $\text{km}2^{1/2}$ kutoka Sengerema Mjini kata ya Nyampulukano wilaya ya Sengerema Mkoani Mwanza. Kutokea stendi kuu ya mjini Sengerema waweza kufika shuleni kwa tekisi Tshs 3,000/= au pikipiki Tshs 1,000/=.

MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

1.0 ADA NA MICHANGO YA SHULE

1.1 Ada ya shule ni Tshs 70,000/= kwa mwaka. Ilipwe kwa mkupuo Tshs 70,000/= au Tshs 35,000/= mwanzoni wa kila muhula. Fedha zilipwe kwenye akaunti Na 31601200072 NMB tawi lolote Tanzania. Jina la akaunti Nyampulukano Secondary School Recurrent Account.

1.2 Michango ya shule

Fedha za michango ya shule zilipwe kwenye akaunti Na 31602300144 tawi lolote Tanzania Jina ni Elimu ya Kujitegemea Nyampulukano sekondari.

***HAIRUHUSIWI KUJA NA SIMU SHULENI**

1.3 Fedha kwa ajili ya michango mbalimbali.

Tahadhari (hazitarudishwa)	10,000/=
Kitanda	55,000/=
Taaluma kwa mwaka	10,000/=
Matibabu kwa mwaka	20,000/=
Ulinzi kwa mwaka	10,000/=
Kitambulisho na nembo	10,000/=
Matengenezo	20,000/=
Wapishi	30,000/=
Daftari la matokeo	3,000/=
Jalada (<i>flat file</i>) la kumbukumbu za mwanafunzi	1,500/=
Gharama ya Maji	10,000/=
Gharama ya Umeme	10,000/=
Remedial	10,000/=
Graduation	5,000/=
JUMLA	204,500/=

1.4 SARE YA SHULE

Suruali 2 kwa wavulana (Zinapatikana shuleni).	27,000/=
Suruali 2 kwa wavulana kwa kazi za nje ya darasa (Zinapatikana shuleni).	27,000/=
Sketi 2 kwa wasichana (Zinapatikana shuleni).	27,000/=
Sketi 2 kwa wasichana kwa kazi za nje ya darasa (Zinapatikana shuleni).	27,000/=
T-shirt 2 zenye ukosi kwa matumizi baada ya vipindi vya darasani.	20,000/=
Tai	3,000/=
T – shirt za michezo 1	7,000/=
Sweta 1	13,000/=
Godoro (3' x 2.5" x 6') kwa WAVULANA <i>super banco</i> 40,000/= au <i>Malaika</i> 20,000/=	
Godoro (3' x 3" x 6') kwa WASICHANA <i>super banco</i> 60,000/= au <i>Malaika</i> 33,000/=	
JUMLA (bila godoro)	97,000/=

❖ Magodoro yanapatikana hapa shuleni.

❖ Taa ya *solar* inaruhusiwa.

1.5 Shule haipokei fedha taslimu. Fedha zote zilipwe kwa kupitia Benki ya NMB, tawi lolote, kwa kutumia namba za akaunti husika na stakabadhi za malipo (Bank pay-in-slips) zenye jina la mwanafunzi ziletwe shuleni siku ya kuripoti. Mwanafunzi hatapokewa shuleni endapo hatakamilisha jumla ya fedha zote kama ilivyoainishwa katika jedwali hapo juu.

2.0 MAHITAJI MENGINE

2.1 Mabunda mawili (2) ya karatasi *Double AA*.

2.2 Bukta 1 rangi ya bluu

2.3 Raba za michezo pea moja, rangi nyeupe.

2.4 Mashuka 2 rangi ya bluu bahari kwa wavulana na pinki kwa wasichana.

2.5 Mto na foronya (foronya rangi ya shuka).

- 2.6 Track suit nyeusi yenye michirizi myeupe.
- 2.7 Taulo
- 2.8 Kanga kwa wasichana (jozi moja)
- 2.9 Kandambili jozi moja
- 2.10 Mswaki na dawa ya meno.
- 2.11 Ndoo 1 (Litre 20), na dumu 1 dogo (Litre 5) kwa ajili ya kutunzia maji ya kunywa.
- 2.12 Kijiko, sahani ya shaba, bakuli la shaba na kikombe kwa jili ya uji.
- 2.13 Taa ya betri kwa tahadhali ya umeme ukatika (ISIWE YAKUCHAJI)
- 2.14 Madaftari makubwa (Counter books) angalau kumi (10) au zaidi
- 2.15 Scientific calculator kwa wanafunzi wa sayansi
- 2.16 Blanketi la kujifunika usiku na chandarua rangi ya bahari (*light blue*).
- 2.17 Viatu vyeusi vya ngozi vya kamba pair 2.
- 2.18 Soksi nyeupe zisizo na malembo kwa wasichana na soksi nyeusi zisizo na malembo kwa wavulana.


3.0 VIFAA VYA USAFI

- 3.1 Mfagio wa ndani wenye mpini mrefu (*Soft broom*) 1
- 3.2 Mfagio mgumu wa chooni wenye mpini mrefu (*Hard broom*) 1
- 3.3 Chelewa ndefu ya nje (fagio la wima) 1. Iliyofungwa kwa wire.
- 3.4 *Squeezer* moja (mpira wa kukaushia maji).
- 3.5 Jembe na mpini wake.
- 3.6 Kifutio cha ubaoni kimoja 1 chenye mshikio wa plastiki.

4.0 MAELEKEZO MENGINE

- 4.1 Tarehe ya kufungua shule imeoneshwa hapo juu, ukichelewa kuripoti shuleni ndani ya siku kumi na nne utapoteza nafasi yako.
- 4.2 Uje na nakala ya hati halisi ya uraia au cheti cha kuzaliwa.
- 4.3 Uje na nakala ya hati yako (*results slip*) ya matokeo ya kidato cha NNE.
- 4.4 Uje na barua hii na viambata vyake vyote. Fomu ya uchunguzi wa afya iliyojazwa na daktari, Fomu ya kukubali kujiunga na shule yetu.
- 4.5 Nguo za nyumbani haziruhusiwi, mwanafunzi atavaa sare za shule muda wote awapo shuleni.
- 4.6 Kila mzazi /mlezi anapaswa kugharamia usafiri wa mwanae kuja shuleni na kurudi nyumbani wakati wa likizo na kumpa fedha za kutosha kwa ajili ya matumizi. Mzazi unakumbushwa kuwa kumpa mwanao fedha inayopita kiasi kwaweza kuchangia kuporomoka kwa elimu yake. Ruhusa ya kufuata fedha za matumizi haitolewi.
- 4.7 Mwanafunzi haruhusiwi kumiliki simu akiwa shuleni. (HARUHUSIWI KUJA NA SIMU SHULENI)
- 4.8 Asiyetimiza maelekezo tajwa hapo juu hatapokewa.

KARIBU SANA



J.M.MARTIN

(MKUU WA SHULE)

MAKUU WA SHULE
 TRAMPOLINANO SHULE YA SEKONDARI
 S.L.P. 104
 SENORREMA

1.0 SHERIA NA KANUNI ZA SHULE HII;

1.1 Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu. Aidha inazingatia miongozo yote inyotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo yote ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa na utapewa nakala mara baada ya kuripoti shuleni.

- a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima, mwanafunzi hatakiwi kutumia lugha chafu kwa walezi na kwa wanafunzi wenzake.
- b) Kutii wito, kuheshimu ofisi za shule, mali binafsi na mali ya umma. Kutofanya hivyo nikosa.
- c) Uwapo shuleni unaruhusiwa kuvaa nguo za shule tu. Nguo za nyumbani hazitakiwi
- d) Kuhudhuria shuleni ni lazima, vipindi vyote ndani na nje ya darasa.
- e) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule.
- f) Taaruma ipewe kipaumbele, hivyo uzembe katika masomo hautavumiliwa.
- g) Kuzingatia ratiba ya shule darasani, bwaloni, mazingira ya usafi, kazi mradi, bwenini na paredi.
- h) Lugha ya mawasiliano ni kiingereza. Kila mwanafunzi ajitahidi kujifunza kwa bidii na kujizoesha kuongea kiingereza.
- i) Mgeni atakaye kutembelea sharti apate kibali kutoka katika uongozi wa shule. Ni marufuku kumtembeza mgeni yeyote katika maeneo ya shule bila kibali cha uongozi wa shule.
- j) Mawasiliano yapitie kwa walezi.
- k) Nywele zisizidi 0.5cm na ndevu zinyolewe wakati wote.
- l) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
- m) Huruhusiwi kwenda kwenye nyumba za walimu bila idhini.

1.2 Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa shule;-

- i) Wizi wa aina yoyote.
- ii) Uasherati na ushoga.
- iii) Ubakaji
- iv) Ulevi na matumizi ya dawa za kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kuberi n.k
- v) Kupiga ama kupigana.
- vi) Kudharau bendera ya taifa.
- vii) Kuoia ama kuolewa.
- viii) Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule.
- ix) Kutoa mimba.
- x) Kugoma, kuchochea na kuongoza migomo au kuvuruga amani na usalama wa shule.
- xi) Kukataa adhabu kwa makusudi.
- xii) Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi.
- xiii) Kuonekana kwenye nyumba za sitarehe na kumbi mbalimbali mfano: Nyumba za kulala wageni na baa.
- xiv) Kuwa na pasi ya umeme, jiko la umeme na vifaa vingine vinavyoweza kusababisha ajali ya moto.
- xv) Kukamatwa na simu shuleni.

2.0 Mambo mengine muhimu;

1. Medical examination form, ijazwe na Mganga wa Hospitali ya serikali.
2. Fomu ya taarifa muhimu, ijazwe kikamilifu na kusainiwa na mzazi na mwanafunzi
3. Fomu ya mkataba wa kutokushiriki migomo, fujo na makosa ya jinai, ijazwe na kusainiwa na mzazi na mwanafunzi.
4. Ulete kivuli cha cheti cha kuzaliwa.

NB. Tafadhali fomu hizi ziletwe siku ya kuripoti shuleni.

MOTO WA SHULE: ELIMU KWA MAENDELEO


WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI

SHULE YA SEKONDARI NYAMPULUKANO

FOMU YA MAELEKEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI PAMOJA NA AHADI YA UTII WA SHERIA ZA SHULE

1. Jina kamili (Kama ilivyo kwenye *Sel-Form*)
2. Anwani ya nyumbani S.L.P WILAYA
3. Tarehe ya kuzaliwa
4. Mahali ulipozaliwa, Kijiji Kata Tarafa
5. Mahali unapoishi kwa sasa WILAYA
6. Shule ya sekondari ulikotoka Anwani
7. Dini/Dhehebu Kabila
8. Jamaa katika familia ambao wanaweza kupelekewa taarifa zako muhimu kwa masuala yahusuyo shule:
 - (i) Jina la Baba Namba ya simu Hai /Si hai
(kama hai) kazi yake Anwani
 - (ii) Jina la mama Namba ya simu Hai /Si hai
(kama hai) kazi yake Anwani
 - (iii) Jina la Mlezi Uhusiano Namba ya simu
kazi yake Anwani S.L.P WILAYA

NB: BANDIKA PICHA ZA WANAOHUSIKA HAPO JUU KWENYE VIBOMA



Mimi (Mwanafunzi) nathibitisha kuwa taarifa nilizojaza hapo juu ni za kweli. Ahadi yangu nakubali kwa dhati kabisa nafasi niliyopewa na Taifa kujiunga na shule hii na ninaahidi kufuata sheria na taratibu zote za shule kama zilivyotolewa na zitakavyotolewa na uongozi wa shule.

.....
Sahihi ya Mwanafunzi

.....
Tarehe

Mimi (Jina la Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi) ambaye ni Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi nimeyasoma masharti na sheria za shule ya Sekondari Nyampulukano ambako kijana wangu amechaguliwa kujiunga. Naahidi kwamba nitamhimiza mwanangu kufuata sheria na taratibu zote za shule kama zilivyoielezwa. Aidha, naahidi kushirikiana na uongozi katika malezi bora ya mwanangu ili baadaye awe raia bora na mwema wa Taifa letu.

.....
Sahihi ya Mzazi/Mlezi

.....
Tarehe

PRIME MINISTER'S OFFICE
REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
SENGEREMA DISTRICT COUNCIL

NYAMPULUKANO SECONDARY SCHOOL

MEDICAL EXAMINATION FORM

(TO BE COMPLETED BY MEDICAL OFFICER IN RESPECT OF ALL FORM I ENTRANTS)

Student's full name.....

Age.....years sex.....

Stool examination.....

Urinalysis.....

Blood count(red &white).....

Syphilis test.....

Spleen.....

Mental condition.....

Sight.....

Chest (T.B).....

Pregnancy

ADDITIONAL INFORMATION (e.g physical defects, impairments or chronic disease requiring special treatment/attention)

.....
.....
.....
.....
.....

I certify that I have examined the above student and recommend that he/she is fit/unfit to pursue his/her secondary education studies

Signature.....

Designation.....

Official stamp.....

Date.....

OFISI YA WAZIRI MKUU
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA SENGEREMA
NYAMPULUKANO SHULE YA SEKONDARI

FOMU YA MKATABA WA KUTOSHIRIKI KATIKA MIGOMO, FUJO NA MAKOSA YA JINAI

Mimi _____ wa kidato cha _____ mwaka _____
ninaahidi kwamba, nitakuwa mwaminifu katika muda wangu wote wa masomo katika
shule hii kwa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai. Pia naahidi kuwa
nitakuwa mwaminifu kwa uongozi wa shule na jumuiya nzima ya Nyampulukano
Sekondari, huku nikifuata sheria na kanuni za shule kwa mujibu wa wizara ya Elimu.

Saini ya Mwanafunzi _____

Tarehe _____

Saini ya Mzazi/Mlezi _____

Tarehe _____